*Mulika, Na. 41 (2), 206-220*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Utabirifu wa Kisemantiki wa Mofimu {Ji-} katika Vitenzi vya Kiswahili

*Maria Gores*[1]
Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na41t2.6

**Ikisiri**

Mofimu ni kipashio cha kimofolojia kinachobeba dhima za kisemantiki. Dhima hizo hutofautiana kutoka mofimu moja na nyingine kama mazingira ya utokeaji wa mofimu yanavyotofautiana. Katika lugha ya Kiswahili, baadhi ya vitenzi huwa na tabia ya kupachikwa mofimu ambazo hubeba dhima tofauti (Khamisi, 1985; Mgullu, 1999; McCarthy 2002; kwa kutaja wachache). Makala haya yanakusudia kuchunguza utabirifu wa kisemantiki wa mofimu {ji-] katika baadhi ya vitenzi vya Kiswahili ili kuona kama ni mara zote mofimu hiyo ikiambatana na vitenzi hivyo tunaweza kutabiri maana. Data iliyochambuliwa imekusanywa kutoka katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la tatu) na *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (Toleo la pili), kwa kutumia mbinu ya usampulishaji nasibu tabakishi, usampulishaji nasibu taratibishi na usampulishaji nasibu ulo rahisi. Katika Makala haya tumeanza kwa kuangazia mbinu zinazobainisha vitenzi vyenye mofimu {ji-} katika kamusi teule za Kiswahili. Pia, tumefafanua utabirifu wa kisemantiki wa mofimu {ji-} katika vitenzi vya Kiswahili. Vilevile, tumeelezea mazingira yanayosababisha utabirifu wa kisemantiki wa mofimu {ji-} katika vitenzi vya Kiswahili. Ili kufikia malengo hayo, Nadharia ya Maana kama Matumizi imetumika. Kwa kuhitimisha, makala haya yametoa mapendekezo kadhaa kuhusu kufanyika kwa uchunguzi zaidi katika kipengele cha mofimu.

## 1.0 Utangulizi

Dhana ya mofimu imejadiliwa na wataalamu mbalimbali. Mathalani, Rubanza (1996), Kreidler (2002), Katamba na Stonham (2006), Lieber (2009) na TUKI (2014) wanaelekea kufanana katika kufasili mofimu kuwa ni kipashio kidogo chenye maana ya kisarufi au ya kileksika. Kipashio hicho kinaweza kuwa sehemu ya neno au neno zima. Maelezo haya yanashabihiana na McCarthy (2002) anaposema kwamba, kila neno linajumuisha sehemu zinazojitosheleza ambapo maana ya kila sehemu ya neno huweza kuamua maana ya neno zima. Kutokana na

[1] **Baruapepe:** mariagoress@gmail.com

maelezo yaliyotolewa na mtaalamu huyu, inaonekana kwamba neno hujumuisha sehemu ndogo ambazo ni mofimu na hizo huwa na maana ambayo huweza kusababisha utabirifu wa kisemantiki. Utabirifu ni hali ya kitu au jambo kuweza kukisiwa kutokana na muktadha au mazingira yaliyopo (Massamba, 2009). Utabirifu wa kisemantiki ni hali ya kuweza kujua maana ya neno kutokana na kuwapo kwa sauti fulani katika neno husika.

Katika kujadili dhima za kisemantiki za mofimu katika lugha ya Kiingereza, McCarthy (2002) anaeleza kwamba ni vigumu kuepuka kuwapo kwa maneno yenye utabirifu wa maana. Ikiwa kuna utabirifu kuntu basi kuna ushawishi wa kuweza kukisia maana kwa mtu anayekutana na neno hilo kwa mara ya kwanza katika mazingira yanayowiana. Anaendelea kueleza kuwa katika lugha ya Kiingereza kuna baadhi ya maneno yenye sauti zinazofanana mwanzoni na huonesha utabirifu wa kisemantiki katika vitenzi. Mathalani, sauti /**sl**/ inapotokea mwanzoni katika vitenzi hutabiri dhana ya ulaini au uchepechepe. Mifano ya vitenzi aliyotoa ni "slip" (ponyoka), "slide" (teleza/nyiririka), "sleek" (lainisha), "slick" (lainisha), na "slaver" (churuza). Maelezo hayo yanatupa mwanga kuwa kuna baadhi ya mofimu ikipachikwa kabla ya shina la neno huleta utabirifu wa kisemantiki katika vitenzi husika. Kwa maneno mengine, tunaweza kusema kwamba, kuwapo kwa mofimu fulani katika baadhi ya maneno kunamsaidia msomaji kuweza kupata maana ya neno hilo kwa urahisi zaidi hata kama ni mara ya kwanza kukutana na neno husika. Hii inatokana na kwamba huenda mofimu iliyopo katika neno au maneno hayo ina ushawishi fulani wa maana, hivyo, inamuwia rahisi msomaji kupata maana.

Mara nyingi mofimu {ji-} inapopachikwa katika vitenzi vya Kiswahili huonesha hali ya kujitendea jambo fulani (Mgullu, 1999). Wesana-Chomi (1989) anasema kuwa kiambishi tenzi {ji-} ni kiambishi awali katika kitenzi. Kiambishi hiki huonesha kwamba mtu au kitu fulani kimejitendea tendo au jambo fulani. Kiambishi {ji-} katika kitenzi hakibadiliki kiumbo kutokana na ngeli au umoja na wingi wa nomino inayohusika. Maelezo ya wataalamu hawa yanaonesha kuwa mofimu {ji-} inapopachikwa katika vitenzi vya Kiswahili huwa na dhima ya kuonesha kwamba kuna ujirejeaji wa nomino kapa ambayo haionekani katika kitenzi husika. Kwa mantiki hiyo, msomaji anapokutana na mofimu {ji-} katika kitenzi chochote anaweza kuihusisha na dhana ya ujirejeaji.

Kitu ambacho tunapaswa kukichunguza kwa makini ili kupata uthibitisho ni kwamba mofimu {ji-} inapojitokeza katika kitenzi chochote cha Kiswahili, je, inaonesha hali ya kujitendea jambo lilelile lililogusiwa na kitenzi kabla ya kupachikwa mofimu hiyo au imevuka mipaka hiyo? Hivyo basi, licha ya kwamba mofimu {ji-} inaonesha hali ya kijitendea jambo, bado maana ya kitenzi kipya kilichoundwa huwa tofauti na kitenzi cha awali. Kwa maana hiyo, kuwapo kwa mofimu {ji-} katika vitenzi vya Kiswahili kunaweza kusaidia kuonesha utabirifu wa kisemantiki. Swali ni je, msomaji anapokutana na mofimu {ji-} katika kitenzi

chochote cha Kiswahili aihusishe na hali ya kujitendea jambo au la? Hali hii ndiyo imemsukuma mtafiti kutaka kutafiti juu ya utabirifu wa kisemantiki wa mofimu {ji-} katika vitenzi vya Kiswahili vilivyopo katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (Toleo la 3),* (kuanzia sasa KKS3) na *Kamusi Kuu ya Kis*wahili (Toleo la 2), (kuanzia sasa KKK2) namna inavyoleta utabirifu wa kisemantiki katika vitenzi vilivyoambishwa mofimu hiyo. Katika sehemu inayofuata tutaangazia mbinu zilizotumika kubainisha vitenzi vya Kiswahili vyenye mofimu {ji-} katika kamusi teule.

## 2.0 Mbinu Zinazobainisha Vitenzi vya Kiswahili vyenye Mofimu {ji-} katika KS3 na KKK2

Katika makala haya tumeanza kwa kubainisha mbinu zilizotumika kudhihirisha vitenzi vyenye mofimu {ji-} katika kamusi teule za Kiswahili. Lengo la kufanya hivi ni kuweza kufahamu kuwa si vitenzi vyote vyenye mofimu hiyo vimeweza kushughulikiwa katika andiko hili. Mbinu hizi zimepatikana kwa kuangalia matumizi ya maneno hayo katika KKS3 na KKK2 na zimefafanuliwa katika kipengele kinachofuata kama ifuatavyo.

### 2.1 Mbinu ya Kileksikografia

Mbinu ya kileksikografia inahusu kuangalia kama vitenzi vya Kiswahili vyenye mofimu {ji-} ikiwa havina mofimu hiyo vyote vinapatikana katika kamusi teule. Mbinu hii imetumika kubainisha vitenzi vya Kiswahili vyenye mofimu {ji-} kwa kuangalia vitenzi vyenye mofimu hiyo kama vinatumika na vidahizo vingine ambavyo vimeingizwa katika kamusi bila mofimu hiyo. Kwa maneno mengine, tunaweza kusema kwamba ikiwa kitenzi cha Kiswahili chenye mofimu {ji-}, shina lake kabla halijawekewa mofimu {ji-} nalo ni kidahizo tofauti katika kamusi hizo teule (yaani kabla ya kupachikwa mofimu hiyo), basi kitenzi hicho kitakuwa kimepachikwa mofimu {ji-} wala {ji-} si sehemu ya kitenzi hicho. Kutokana na mbinu ya kileksikografia, tunaweza kupata vitenzi mbalimbali vyenye mofimu {ji-}. Hapa tumeonesha baadhi ya vitenzi hivyo katika Jedwali Na. 1 lifuatalo kama mifano.

***Jedwali Na. 1: Vitenzi vya Kiswahili vyenye Mofimu {ji-} Vilivyobainishwa kwa Kutumia Mbinu ya Kileksikografia***

| Na. | Vitenzi bila Mofimu {ji-} na Maana zake | Vitenzi vyenye Mofimu {ji-} na Maana zake |
|---|---|---|
| 1. | **Komba**<br>**Maana:** ondoa sehemu ya kitu k.v. asali, chakula au mchuzi kutoka kwenye bakuli au chungu kwa kupitisha kidole. | **Jikomba**<br>**Maana:** jitafutia masilahi kwa kujipendekeza kwa wenye uwezo. |
| 2. | **Vuna**<br>**Maana:** ondoa mazao k.v. matunda au mahindi shambani baada ya kukomaa. | **Jivuna**<br>**Maana:** hisi kuwa una zaidi kuliko wengine; jiona bora. |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | **Nyonga**<br>**Maana: i.** toa uhai wa mtu au mnyama kwa kutundika kamba shingoni, kusokota shingo. | **Jinyonga**<br>**Maana:** jifunge kamba au kitu chochote kinachoweza kufunga shingoni agh. kwa lengo la kujitoa uhai. |
| 4. | **Buruza**<br>**Maana:** vuta kwa kufanya msuguo. | **Jiburuza**<br>**Maana:** tembea kwa kujilazimisha. |
| 5. | **Tetea**<br>**Maana:** simamia mtu ili kumkinga na mambo, agh. mabaya yaliyomfika. | **Jitetea**<br>**Maana:** toa kauli mbele za watu kuonyesha kuwa hukufanya kitu fulani au kwa kusudi ya kufanyiwa jambo. |

**Chanzo:** Data ya **KKS3** na KKK2 (2018)

Jedwali Na. 1 hapo juu linaonesha mifano ya vitenzi vya Kiswahili vyenye mofimu {ji-} vilivyobainishwa kwa kutumia mbinu ya kileksikografia pamoja na maana zake katika KKS3 na KKK2. Tukichunguza kwa makini mifano hiyo iliyotolewa katika jedwali hapo juu inaonesha kuwa vitenzi vyenye mofimu {ji-} vina vidahizo vingine ambavyo havina mofimu hiyo na vimeorodheshwa katika kamusi kama vidahizo tofauti. Hii ina maana kwamba {ji-} iliyopo katika vitenzi hivyo ni mofimu, wala si sehemu ya kitenzi husika.

## 2.2 Mbinu ya Ujazo wa Kisemantiki

Ujazo wa kisemantiki ni hali ya neno kujitosheleza kimaana. Mbinu hii inaangalia kama mofimu {ji-} ikiondolewa katika kitenzi husika maana inaweza kupatikana katika sehemu ya kitenzi hicho iliyobakia. Hivyo, tunaweza kusema kwamba ikiwa sehemu ya kitenzi bado ina ujazo wa kisemantiki baada ya kuondolewa mofimu {ji-}, basi mofimu hiyo imepachikwa katika kitenzi husika, hivyo, si sehemu ya kitenzi hicho. Vitenzi vinavyobainishwa kwa kutumia mbinu hii, mara nyingine mashina yanayobakia baada ya kuondolewa mofimu {ji-} huweza kuwa hayajaorodheshwa katika kamusi ili kuyabaini kama ni maneno yenye mofimu {ji-} licha ya kuwa yana ujazo wa kisemantiki. Tutazame baadhi ya mifano ya vitenzi vyenye mofimu {ji-} vinavyoweza kubainishwa kwa kutumia mbinu ya ujazo wa kisemantiki.

***Jedwali Na. 2: Vitenzi vya Kiswahili vyenye Mofimu {ji-} Vilivyobainishwa kwa Kutumia Mbinu ya Ujazo wa Kisemantiki***

| Na. | Vitenzi vyenye Mofimu {ji-} | Maana za Vitenzi vyenye Mofimu {ji-} |
|---|---|---|
| 1. | Jilia | **Maana**: **i.** kula bila kuchukua tahadhari.<br>**ii.** kula bila kusaidiwa na mtu. |
| 2. | Jiamulia | **Maana:** fanya uamuzi mwenyewe bila ya kushawishiwa au kushirikisha mtu yeyote. |
| 3. | Jitambulisha | **Maana:** julisha mtu taarifa muhimu kama vile jina, unakotoka na shughuli zako ili akufahamu vizuri. |
| 4. | Jisemea | **Maana: i.** toa maneno ovyoovyo bila kujali athari ya kile usemacho. |

| | | |
|---|---|---|
| | | **ii.** jitetee kuondokana na tuhuma au jambo unalodaiwa kufanya. |
| 5. | Jizalia | **Maana:** zaa bila mpangilio. |

**Chanzo:** Data ya KKS3 na KKK2 (2018)

Jedwali Na. 2 linaonesha mifano ya vitenzi vya Kiswahili vyenye mofimu {ji-} vilivyobainishwa kwa kutumia mbinu ya ujazo wa kisemantiki. Katika mifano hiyo tunaona kuwa maneno yaliyobainishwa yamepachikwa mofimu {ji-} na yamepewa maana zake tulizoziorodhesha katika jedwali hilo. Maneno hayo yanapoondolewa mofimu {ji-} hubaki mashina ambayo yanajitosheleza kimaana lakini mashina hayo hayajaingizwa katika kamusi kama vidahizo vinavyojitegemea na kutolewa ufafanuzi. Licha ya mashina hayo kutoingizwa na kutotolewa ufafanuzi katika kamusi hizo mbili, bado yana ujazo wa maana kulingana na matumizi yake.

## 3.0 Utabirifu wa Kisemantiki wa Mofimu {ji-} katika Vitenzi vya Kiswahili

Baada ya kuchunguza mbinu zilizotumika kubainisha vitenzi vya Kiswahili vyenye mofimu {ji-} katika kamusi teule, sasa tunafafanua utabirifu wa kisemantiki wa mofimu {ji-} katika vitenzi teule vya Kiswahili. Ili kufafanua utabirifu huu, hojaji thelathini zilizoandikwa vitenzi vya Kiswahili kabla na baada ya upachikaji wa mofimu {ji-} pamoja na maana zake ziliandaliwa kisha kupelekwa uwandani. Vitenzi hivyo viliteuliwa kutoka katika KKS3 na KKK2 kwa kutumia mbinu ya usampulishaji nasibu taratibishi. Hapa watoataarifa walitakiwa kuhakiki maana zote za vitenzi zilizotolewa na kama kuna maana za ziada ambazo hazikuorodheshwa katika vitenzi husika waziongeze katika nafasi zilizoachwa wazi. Vilevile, walitakiwa kuonesha ni vitenzi vipi vina utabirifu wa kisemantiki kwa maana kuwa ni vitenzi vipi maana yake inaweza kutabirika kwa kuangalia shina la vitenzi hivyo kabla ya kuwekewa mofimu {ji-} na baada ya kuwekewa mofimu hiyo.

Baada ya watoataarifa kuhakiki vitenzi teule vya Kiswahili, waliona kuwa maana zote zilizopo katika hojaji ndizo wanazozifahamu, hivyo, wakakubaliana nazo kuwa ni sahihi. Katika kuonesha utabirifu wa kisemantiki, watoataarifa walidai kuwa kuna vitenzi ambavyo maana zake zinatabirika na vitenzi vingine maana zake hazitabiriki kutokana na kupachikwa mofimu {ji-} katika vitenzi husika.

### 3.1 Vitenzi vya Kiswahili Vinavyoonesha Utabirifu wa Kisemantiki kutokana na Kupachikwa Mofimu {ji-}

Baada ya watoataarifa kuhakiki vitenzi vilivyoteuliwa kutoka katika KKS3 na KKK2 waliona kuwa kuna baadhi ya vitenzi hivyo ambavyo maana zake hutabirika kutokana na kupachikwa kwa mofimu {ji-} katika vitenzi husika. Hapa tumeangalia mifano michache ya vitenzi hivyo kama ifuatavyo:

***Jedwali Na. 3: Vitenzi vya Kiswahili Vinavyoonesha Utabirifu wa Kisemantiki baada ya Kupachika Mofimu {ji-}***

| Na. | Vitenzi bila Mofimu {ji-} na Maana zake | Vitenzi vyenye Mofimu {ji-} na Maana zake |
|---|---|---|
| 1. | **Amua**<br>**Maana:** kata shauri kuhusu jambo au mambo fulani. | **Jiamulia**<br>**Maana:** fanya uamuzi mwenyewe bila ya kushawishiwa au kushirikisha mtu yeyote. |
| 2. | **Aibisha**<br>**Maana:** tendea mtu kitu au jambo la kumfedhehesha; vunjia heshima. | **Jiaibisha**<br>**Maana:** fanya jambo la aibu litakaloshusha hadhi yako katika jamii. |
| 3. | **Furahisha**<br>**Maana:** fanya jambo la kumtia mtu furaha. | **Jifurahisha**<br>**Maana:** fanya mambo yanayokupa furaha moyoni. |
| 4. | **Mudu**<br>**Maana:** kuwa na uwezo, nguvu na maarifa ya kufanya jambo. | **Jimudu**<br>**Maana:** jaliwa uwezo wa kutekeleza jambo bila ya msaada wowote. |
| 5. | **Kama**<br>**Maana:** minya kiungo cha kiumbe ili kutoa kimiminika kilichomo ndani agh, wakati wa kutoa maziwa ya mnyama; kamua. | **Jikama**<br>**Maana:** kakamaa mwili kwa kutumia nguvu za misuli ya mwili wako kama ufanyavyo unaposukuma haja kubwa. |

**Chanzo**: Data ya KKS3 na KKK2 (2018)

Jedwali Na. 3 linaonesha vitenzi vya Kiswahili ambavyo havijapachikwa mofimu {ji-} na vilivyopachikwa mofimu {ji-} ili kuonesha jinsi mofimu {ji-} inavyotabiri maana ya kitenzi baada ya kuweka mofimu hiyo. Lengo hasa ni kuonesha kwamba baada ya kupachikwa kwa mofimu hiyo maana ya kitenzi husika inahusiana na maana ya kitenzi hicho kabla ya kupachika mofimu hiyo. Kutokana na mifano tajwa hapo juu, tunaona kwamba kupachikwa kwa mofimu {ji-} katika shina la kitenzi kunamsaidia msomaji kutabiri maana ya kitenzi husika.

## 3.2 Vitenzi vya Kiswahili Visivyoonesha Utabirifu wa Kisemantiki kutokana na Kupachikwa Mofimu {ji-}

Baada ya kuangalia mifano ya vitenzi vya Kiswahili ambavyo vinaonesha utabirifu wa kisemantiki kutokana na kupachikwa kwa mofimu {ji-} pamoja na ufafanuzi wake, vilevile watoataarifa waliona kuwa kuna baadhi ya vitenzi havina utabirifu wa kisemantiki baada ya kupachika mofimu hiyo. Vitenzi hivyo ni vile ambavyo maana inayopatikana baada ya kitenzi kupachikwa mofimu {ji-} haifanani na maana ya shina la vitenzi hivyo kabla havijapachikwa mofimu hiyo. Miongoni mwa vitenzi hivyo vinapatikana katika Jedwali Na. 4 lifuatalo:

***Jedwali Na. 4: Vitenzi vya Kiswahili Vinavyoonesha Kutokuwapo kwa Utabirifu wa Kisemantiki baada ya Kupachika Mofimu {ji-}***

| Na. | Vitenzi bila Mofimu {ji-} na Maana zake | Vitenzi vyenye Mofimu {ji-} na Maana zake |
|---|---|---|
| 1. | **Sikia**<br>**Maana: i.** pokea mawimbi ya sauti kwa kutumia sikio;<br>**ii.** fuata amri; tii;<br>**iii.** kuwa na hisi fulani; | **Jisikia**<br>**Maana: i.** kuwa katika hali fulani:<br>**ii.** jiona bora kuliko –ingine. |
| 2. | **Dai**<br>**Maana: i.** taka urejeshewe kitu chako ulichompatia mtu mwingine kwa makubaliano ya kurudishiwa; wia.<br>**ii.** toa kauli ya kuonyesha msimamo kuhusu jambo fulani. | **Jidai**<br>**Maana:** jipa hali au sifa isiyo yako; jikweza. |
| 3. | **Pendekeza**<br>**Maana: i.** shawishi wazo kwa watu agh. katika mikutano ili walijadili na kuliunga mkono.<br>**ii.** fanya watu wapende kitu au jambo. | **Jipendekeza**<br>**Maana:** kuwa karibu na mtu, kumsifia, kumsaidia, kumpa taarifa au zawadi kwa lengo la kushawishi kupata upendeleo kutoka kwake. |
| 4. | **Tanda**<br>**Maana: i.** fuma kamba kutoka mfumbati mmoja wa kitanda hadi mwingine ili kutengeneza sehemu ya katikati kwa ajili ya kulalia.<br>**ii.** vua samaki au dagaa kwa kutumia wavu au nguo. | **Jitanda**<br>**Maana:** jifunika kichwani au mabegani nguo k.v. kanga, mtandio au kitenge. |
| 5. | **Ona**<br>**Maana: i.** angalia na kutambua kitu kwa macho; tazama<br>**ii.** tambua kitu kwa hisia agh. za ngozi; hisi. | **Jiona**<br>**Maana:** kuwa na mazoea ya kuringa na kujivuna. |

**Chanzo:** Data ya KKS3 na KKK2 (2018)

Jedwali Na. 4 linaonesha vitenzi vya Kiswahili kabla na baada ya kupachikwa mofimu {ji-}. Katika jedwali hili tumeonesha mifano ya vitenzi vya Kiswahili kabla ya kupachikwa mofimu {ji-} na baada ya kupachikwa mofimu hiyo. Mifano hiyo inaonesha kwamba kabla ya kupachikwa kwa mofimu hiyo maana ya kitenzi husika ilikuwa tofauti na baada ya kupachikwa mofimu hiyo maana ikawa tofauti pia. Kutokana na mifano tajwa hapo juu, data iliyopatikana inaonesha kuwa kupachikwa kwa mofimu {ji-} katika shina la kitenzi hakumsaidii msomaji kutabiri maana ya kitenzi husika, yaani maana ya kitenzi kabla ya kupachika mofimu {ji-} haina uhusiano hata kidogo na maana ya kitenzi hicho baada ya kupachika mofimu hiyo. Hali hii inatokana na ukweli kwamba mofimu {ji-} haina mchango wowote wa kimaana katika kitenzi husika japokuwa sehemu ya kitenzi kabla ya kupachikwa mofimu hiyo zinafanana. Hivyo, kutokana na data tuliyokusanya katika makala haya inaoneha kuwa kuwapo kwa mofimu {ji-} katika baadhi ya vitenzi vya Kiswahili si msaada kwa msomaji kuweza kutabiri maana ya kitenzi husika.

## 4.0 Mazingira Yanayosababisha Utabirifu wa Kisemantiki wa Mofimu {ji-} katika Vitenzi vya Kiswahili

Katika kuelezea mazingira yanayosababisha utabirifu wa kisemantiki wa mofimu {ji-} katika vitenzi vya Kiswahili vyenye mofimu {ji-} vilivyobainishwa kwa kutumia mbinu ya kileksikografia na mbinu ya ujazo wa kisemantiki tumeweza kubainisha mazingira kadhaa. Mazingira haya yamepatikana baada ya kuchunguza vitenzi vya Kiswahili vinavyoonesha utabirifu wa kisemantiki kwa kupachikwa mofimu {ji-}. Mazingira hayo tutayaelezea kama ifuatavyo:

### 4.1 Mazingira ya Kimofolojia

Kutokana na data tuliyokusanya kutoka katika KKS3 na KKK2 inaonekana kuwa miongoni mwa mazingira yanayosababisha utabirifu wa kisemantiki wa mofimu {ji-} katika vitenzi vya Kiswahili ni mazingira ya kimofolojia. Mazingira haya yamegawanyika katika makundi mbalimbali ambayo ni: kunyambuliwa kwa vitenzi vya Kiswahili kabla na baada ya kupachikwa kwa mofimu {ji-} pamoja na ukopaji wa maneno (vitenzi) kutoka katika lugha nyingine. Ufafanuzi wa makundi hayo umetolewa katika sehemu inayofuata kama ifuatavyo.

#### 4.1.1 Kunyambuliwa kwa Vitenzi

Vitenzi vya Kiswahili vilivyopachikwa mofimu {ji-} ambavyo vimenyambuliwa vinaonekana kuwa na utabirifu wa kisemantiki wa mofimu {ji-} kwa kiasi kikubwa tofauti na vile ambavyo havijanyambuliwa japokuwa baadhi ya vitenzi ambavyo havijanyambuliwa huonesha utabirifu huo. Mathalani, tukichunguza data tuliyokusanya kutoka katika KKS3 na KKK2, imebainika kuwa karibu vitenzi vyote ambavyo vimenyambuliwa ndivyo vinavyoonesha utabirifu wa kisemantiki wa mofimu {ji-} katika vitenzi husika. Katika mazingira haya ya kimofolojia ya kunyambuliwa kwa vitenzi, ikumbukwe kwamba kuna baadhi ya vitenzi ambavyo kwa asili yake vimenyambuliwa kutoka katika kategoria nyingine ya maneno hasa nomino wakati kuna baadhi ya vitenzi vingine ambavyo vimenyambuliwa kwa kuongeza kauli fulani katika kitenzi husika. Jambo la kuzingatia hapa ni kwamba mara nyingi unyambulishaji hubadili kategoria ya neno na mara chache kutokubadili kategoria ya neno.

##### 4.1.1.1 Kunyambuliwa kwa Vitenzi kutoka katika Kategoria nyingine ya Maneno

Katika unyambulishaji huu tunaona kwamba kuna baadhi ya vitenzi vya Kiswahili vyenye mofimu {ji-} ambavyo vimenyambuliwa na kuweza kuonesha utabirifu wa kisemantiki. Kutokana na data tuliyokusanya kutoka katika KKS3 na KKK2, imebainika kuwa vitenzi hivyo vilivyonyambuliwa vimetoka katika kategoria nyingine ya maneno ambayo ni nomino. Tunaweza kuangalia baadhi ya mifano ya vitenzi hivyo katika Jedwali Na. 5 lifuatalo.

***Jedwali Na. 5: Vitenzi Vilivyonyambuliwa kutoka katika Kategoria nyingine ya Maneno (Nomino)***

| Na. | Nomino Zilizonyambuliwa na Maana zake | Vitenzi Vilivyopatikana baada ya Kunyambuliwa na Maana zake | Vitenzi vyenye Mofimu {ji-} na Maana zake |
|---|---|---|---|
| 1. | **Bidii** **Maana:** ari ya kufanya jambo. | **Bidiisha** **Maana:** hamasika kutekeleza jambo fulani. | **Jibidiisha** **Maana:** weka juhudi zaidi katika kufanya jambo. |
| 2. | **Aibu** **Maana:** Jambo limvunjialo mtu heshima. | **Aibisha** **Maana:** tendea mtu kitu au jambo la kumfedhehesha; vunjia heshima. | **Jiabisha** **Maana:** fanya jambo la aibu litakaloshusha hadhi yako katika jamii. |
| 3. | **Nasaba** **Maana:** uhusiano wa kizazi baina ya watu; uhusiano katoka katika mlango au ukoo mmoja. | **Nasibisha** **Maana:** husisha mtu au kitu na familia, jambo au kitu kingine. | **Jinasibisha** **Maana:** jihusisha na kitu au mtu fulani. |
| 4. | **Shitaka** **Maana:** maelezo ya malalamiko ambayo hupelekwa mbele ya mahakama, baraza au kwa mtu ili kutolewa hukumu kuhusu kitendo alichotendewa mtu, jamii, n.k. kinyume cha sharia au taratibu fulani. | **Shitaki** **Maana:** wasilisha malalamiko dhidi ya mtu, asasi au serikali mbele ya vyombo vya usuluhishi; tafuta haki. | **Jishitaki** **Maana:** toa maneno, onyesha matendo yanayodhihirisha kutenda jambo lisilokubalika, lililo kinyume. |
| 5. | **Taabu** **Maana:** hali ya kutokuwa na raha. | **Taabisha** **Maana:** tia mtu kwenye dhiki, dhikisha; -pa mtu shida. | **Jitaabisha** **Maana:** fanya mwenyewe jambo kwa shida kubwa. |

**Chanzo:** Data ya KKS3 na KKK2 (2018)

Katika Jedwali Na. 5 tumeonesha vitenzi vilivyonyambuliwa kutoka katika kategoria nyingine ya maneno husussani nomino. Vitenzi hivi vinaonesha kuwa kunyambuliwa kwa kitenzi husika huweza kusababisha mazingira rafiki katika kuonesha utabirifu wa kisemantiki wa mofimu {ji-}. Kwa maana hiyo, kutokana na data tuliyokusanya tumeweza kupata mazingira ya kimofolojia ya kunyambuliwa kwa vitenzi hususani kutoka katika kategoria nyingine ya maneno kuwa miongoni mwa mazingira yanayosababisha utabirifu wa kisemantiki katika vitenzi husika. Kwa maneno mengine tunaweza kusema kwamba, vitenzi vyenye mofimu {ji-} vilivyoorodheshwa katika jedwali hapo juu mashina yake yamenyambuliwa kutoka katika kategoria ya nomino kisha kupachikwa mofimu hiyo na kusababisha utabirifu wa kisemantiki.

### 4.1.1.2 Kunyambuliwa kwa Vitenzi katika Kauli ya Kutendea

Mazingira mengine yanayosababisha utabirifu wa kisemantiki wa mofimu {ji-} katika vitenzi vya Kiswahili ni kunyambuliwa kwa vitenzi katika kauli ya kutendea ambayo ina mofimu tofauti zinazoiwakilisha kama vile {-e-}, {-i-}, {-le-}, {-li-} n.k. Kutokana na data tuliyokusanya kutoka katika KKS3 na KKK2 tumeweza kupata baadhi ya vitenzi vya Kiswahili ambavyo vimepachikwa kauli ya kutendea, hivyo, kusababisha utabirifu wa kisemantiki. Vitenzi hivyo vimeoneshwa katika Jedwali Na. 6 lifuatalo:

***Jedwali Na. 6: Vitenzi Vilivyonyambuliwa katika Kauli ya Kutendea***

| **Na.** | **Mashina ya Vitenzi halisi na Maana zake** | **Vitenzi Vilivyopachikwa Kauli ya Kutendea na Maana zake** | **Vitenzi Vyenye Mofimu {ji-} na Maana zake** |
|---|---|---|---|
| 1. | **Toa**<br>**Maana: i.** ondoa kitu kilicho ndani ya kitu kingine, kundi au eneo maalumu.<br>**ii.** fanya kitu au jambo lisikike, lionekane au lifahamike;<br>**iii**. badilisha umilikaji wa kitu cha mtu mmoja ili kiwe cha mwingine;<br>**iv.** punguza idadi ya kitu katika hesabu; kinyume cha jumlisha. | **Tolea**<br>**Maana:** patia mtu kitu k.v. fedha kwa niaba ya mtu fulani. | **Jitolea**<br>**Maana: i.** tenda jambo kwa hiari na bila ujira.<br>**ii.** toa msaada. |
| 2. | **Pata**<br>**Maana:** kuwa na jambo, hali au kitu. | **Patia**<br>**Maana:** -pa, kabidhi. | **Jipatia**<br>**Maana:** fanikiwa kupata kitu fulani baada ya kufanya jitihada k.v. kujifunza kwa bidii au kufanya mazoezi kwa nguvu. |
| 3. | **Kaa**<br>**Maana:** weka makalio au matako juu ya kitu. | **Kalia**<br>**Maana: i.** keti juu ya kitu.<br>**ii.** kaa na jambo bila ya kulifanyia kazi; kwamisha.<br>**iii.** jihusisha na jambo fulani. | **Jikalia**<br>**Maana: i.** kaa na kukosa la kufanya.<br>**ii.** kaa bila ya kufanya kazi. |
| 4. | **Vaa**<br>**Maana:** zingirisha au eneza kitu k.v. nguo au shanga katika sehemu ya mwili. | **Valia**<br>**Maana:** vaa mavazi mazuri ya kupendeza. | **Jivalia**<br>**Maana: i.** vaa bila mpangilio, vaa hobelahobela.<br>**ii.** vaa nguo bila ya kusaidiwa. |
| 5. | **Zaa**<br>**Maana: i.** vyaa mtoto.<br>**ii.** hali ya mmea kutoa maua na kupata matunda. | **Zalia**<br>**Maana:** zaa kwa ajili ya mtu mwingine. | **Jizalia**<br>**Maana:** zaa bila mpangilio. |

**Chanzo:** Data ya KKS3 na KKK2 (2018)

Katika Jedwali Na. 6 tumeonesha vitenzi vilivyonyambuliwa katika kauli ya kutendea ambavyo kutokana na kupachikwa kwa mofimu {ji-} kumesababisha utabirifu wa kisemantiki katika vitenzi husika. Vitenzi hivi vimeweza kupokea mofimu {ji-} baada tu ya kunyambuliwa kwa kupachikwa kauli ya kutendea. Si kwamba vitenzi hivyo visiponyambuliwa haviwezi kuwa na maana, la hasha, bali data tuliyokusanya imeonesha vitenzi hivyo. Hata hivyo, kwa upande mwingine tunaweza kusema kwamba kama vitenzi ambavyo havijanyambuliwa vingepachikwa mofimu {ji-} vingekuwa na ukakasi fulani wa kimaana.

### 4.1.1.3 Kunyambuliwa kwa Vitenzi katika Kauli ya Kutendesha

Kulingana na data tuliyokusanya katika makala haya, kuna baadhi ya vitenzi vilivyopachikwa mofimu {ji-} ambavyo vimenyambuliwa kwa kupachikwa kauli ya kutendesha. Kauli hii huonesha usababishi wa kitenzi, yaani kitendo fulani kimesababishwa kitokee. Katika kauli ya kutendesha kuna mofimu kama vile {-ish-}, {-esh-}, {-z-} n.k. Tuangalie vitenzi vilivyonyambuliwa kwa kupachikwa kauli ya kutendesha na kusababisha utabirifu wa kisemantiki katika vitenzi hivyo katika jedwali lifuatalo.

***Jedwali Na. 7: Vitenzi Vilivyonyambuliwa katika Kauli ya Kutendesha***

| Na. | Mashina ya Vitenzi halisi na Maana zake | Vitenzi Vilivyopachikwa Kauli ya Kutendesha na Maana zake | Vitenzi vyenye Mofimu {ji-} na Maana zake |
|---|---|---|---|
| 1. | **Endelea**<br>**Maana**: **i.** songa mbele.<br>**ii.** zidi kufanya jambo au kitu;<br>**iii.** kutoka katika hali duni kwenda katika hali bora. | **Endeleza**<br>**Maana: i.** fululiza kufanya jambo.<br>**ii.** ongeza elimu.<br>**iii.** taja au andika tahajia ya neno. | **Jiendeleza**<br>**Maana:** fanya juhudi za kujipatia elimu, mali au ustawi. |
| 2. | **Funda**<br>**Maana:** fundisha, hasa mafundisho ya nyumbani; tia unyagoni. | **Fundisha**<br>**Maana: i.** -pa mtu elimu au maarifa ya jambo fulani.<br>**ii.** elekeza mtu au mnyama kufanya jambo fulani. | **Jifundisha**<br>**Maana:** fanya jitihada za kuelewa au kujua jambo fulani bila msaada wa mtu mwingine. |
| 3. | **Furahi**<br>**Maana:** kuwa katika hali ya ukunjufu wa moyo. | **Furahisha**<br>**Maana:** fanya jambo la kupatia mtu furaha. | **Jifurahisha**<br>**Maana:** fanya mambo yanayokupa furaha moyoni. |
| 4. | **Zaa**<br>**Maana: i.** toa mtoto toka tumboni;<br>**ii.** toa matunda kama ifanyavyo mimea. | **Zalisha**<br>**Maana: i.** saidia mwanamke mjamzito au mnyama jike mwenye mimba kuzaa mtoto.<br>**ii.** fanya shughuli za kilimo, ufugaji, biashara na utengenezaji wa bidhaa za viwandani zinazoingiza pato | **Jizalisha**<br>**Maana: i.** jifungua watoto wengi bila mpangilio.<br>**ii.**jifungue mwenyewe bila msaada wa mkunga, muuguzi wala |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | kwa mtu binafsi na taifa kwa ujumla. | madaktari. |
| 5. | **Lala**<br>**Maana**: **i.** kuwa katika usingizi; potewa na fahamu kwa sababu ya kuingiwa na usingizi;<br>**ii.** weka mwili wote chini; jinyoosha k.v. kitandani. | **Laza**<br>**Maana: i.** fanya au peleka mtu akalale usingizi, lalisha.<br>**ii.** hifadhi mgonjwa hospitalini ili atibiwe.<br>**iii.** ibuka mshindi kwenye mchezo. | **Jilaza**<br>**Maana:** pumzika kwa kulala bila kupata usingizi. |

**Chanzo:** Data ya KKS3 na KKK2 (2018)

Vitenzi vya Kiswahili katika Jedwali Na. 7 vimenyambuliwa kwa kupachikwa kauli nyingine ambayo ni ya utendeshi. Katika vitenzi hivyo inaonekana kuwa, upachikaji wa mofimu {ji-} ulihitaji kunyambulishwa kwa vitenzi hivyo ndipo uweze kufanyika barabara. Hivyo basi, mahitaji ya kunyambuliwa kwa vitenzi hivyo ili viweze kupokea mofimu {ji-} yamesababisha kutokea kwa utabirifu wa kisemantiki. Pia, data hii inaonesha kuwapo kwa ulazima wa kunyambulishwa kwa vitenzi hivyo; huenda vitenzi ambavyo vimenyambulishwa vingepachikwa mofimu {ji-} bila kunyambuliwa vingekuwa na uvulivuli wa maana.

### 4.1.2 Ukopaji wa Vitenzi kutoka katika Lugha nyingine

Ukopaji ni mbinu mojawapo miongoni mwa mbinu nyingine za uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili. Katika mbinu hii maneno kutoka lugha nyingine huchukuliwa na kutumika katika lugha nyingine ama kwa kurahisisha maumbo ya maneno husika ili yaendane na maumbo ya maneno katika lugha kopaji au kuchukuliwa maneno kama yalivyo bila kufanyiwa marekebisho yoyote na kutumika katika lugha iliyokopwa. Kutokana na data tuliyokusanya, imebainika kuwa baadhi ya vitenzi vya mkopo vilivyopo katika lugha ya Kiswahili vinapopachikwa mofimu {ji-} husababisha utabirifu wa kisemantiki katika vitenzi husika. Vitenzi hivyo vya mkopo vinavyoweza kusababisha utabirifu wa kisemantiki ni kama vifuatavyo:

***Jedwali Na. 8: Vitenzi Vilivyokopwa kutoka katika Lugha nyingine***

| **Na.** | **Vitenzi Vilivyokopwa na Maana zake** | **Lugha Iliyokopwa** | **Vitenzi vyenye Mofimu {ji-} na Maana zake** |
|---|---|---|---|
| 1. | **Hifadhi**<br>**Maana: i.** tunza kitu kwenye sehemu salama kwa ajili ya kukitumia wakati mwingine.<br>**ii.** tia jambo moyoni. | **Kiarabu** | **Jihifadhi**<br>**Maana:** nenda mahali pa usalama patakapokupa amani na utulivu. |
| 2. | **Fariji**<br>**Maana: i.** –pa mtu utulivu baada ya kuwa katika huzuni.<br>**ii.** furahisha. | **Kiarabu** | **Jifariji**<br>**Maana: i.** fanya kitu ambacho kitakuondolea majonzi k.v. kuburudika kwa muziki, chakula au kinywaji. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | **ii.** fanya kitu ambacho kitakupa matumaini na kukurejeshea nguvu agh. baada ya kupata matokeo mabaya. |
| 3. | **Sitiri**<br>**Maana: i.** funika kitu agh. viungo vya mwili yenye kutia aibu; ficha.<br>**ii.** hifadhi kitu sehemu maalumu agh. kwa ajili ya matumizi ya baadaye.<br>**iii.** kinga au zuia kitu kisipatwe na madhara. | **Kiarabu** | **Jisitiri**<br>**Maana: i.** jilinde juu ya jambo linaloweza kukuletea fedheha.<br>**ii.** jihifadhi kwa nguo maungo ya mwili ili usiwe uchi au kujilinda dhidi ya kitu kingine k.v. baridi, upepo au joto. |
| 4. | **Hadhari**<br>**Maana:** chukua tahadhari katika kufanya jambo; kuwa macho, kuwa makini. | **Kiarabu** | **Jihadhari**<br>**Maana:** kuwa mwangalifu katika jambo. |
| 5. | **Kusuru**<br>**Maana:** fanya jambo kwa kujilazimisha. | **Kiarabu** | **Jikusuru**<br>**Maana:** fanya jitihada katika utekelezaji wa jambo. |

**Chanzo:** Data ya KK3 na KKK2 (2018)

Vitenzi vilivyokopwa kutoka katika lugha nyingine na kutumika katika Kiswahili vimeweza kubainika katika data tuliyoipata kwa ajili ya makala haya. Data yetu imeonesha kuwa vitenzi vyote vilivyokopwa vimetoka katika lugha ya Kiarabu. Kwa maana hiyo, vitenzi hivi vyote vilivyokopwa kisha kupachikwa mofimu {ji-} vimeweza kusababishiwa utabirifu wa kisemantiki.

### 4.2 Mazingira ya Kisemantiki

Katika mazingira ya kisemantiki yanayosababisha utabirifu wa kisemantiki wa mofimu {ji-} tumeonesha kwamba maana ya kitenzi husika kilichopachikwa mofimu {ji-} ndiyo huweza kumsababishia msomaji aweze kupata utabirifu wa kisemantiki. Kwa maneno mengine, tunaweza kusema kwamba msomaji atakapofahamu maana ya kitenzi fulani kilichopachikwa mofimu {ji-} ataweza kutambua kwamba kitenzi hicho kina utabirifu wa maana au la. Tuangalie mifano ifuatayo kwa ufafanuzi zaidi.

***Jedwali Na. 8: Vitenzi Vinavyoonesha Utabirifu wa Kisemantiki kutokana na Mazingira ya Kisemantiki***

| Na. | Vitenzi bila Mofimu {ji-} na Maana zake | Vitenzi vyenye Mofimu {ji-} na Maana zake |
|---|---|---|
| 1. | **Tetea**<br>**Maana:** simamia mtu ili kumkinga na mambo, agh. mabaya yaliyomfika. | **Jitetea**<br>**Maana:** toa kauli mbele za watu kuonyesha kuwa hukufanya kitu fulani au kwa kusudi ya kufanyiwa jambo. |
| 2. | **Banza**<br>**Maana:** weka kitu sehemu nyingine kwa kuficha ili kisionekane kabisa au kwa urahisi. | **Jibanza**<br>**Maana: i.** kaa mahali penye ufinyu wa nafasi.<br>**ii.** kaa mahali kwa lengo la kutoonekana au kujisitiri dhidi ya jambo baya. |
| 3. | **Hisi**<br>**Maana:i.** tambua kwa njia ya ngozi.<br>**ii.** fikiria usahihi wa kitu kwa njia za milango ya fahamu k.v. kuona, kunusa, kugusa, kuonja au kusikia. | **Jihisi**<br>**Maana:** pata ufahamu wa hali iliyomo ndani ya mwili wako. |
| 4. | **Kama**<br>**Maana:** minya kiungo cha kiumbe ili kutoa kimiminika kilichomo ndani agh. wakati wa kutoa maziwa ya mnyama; kamua. | **Jikama**<br>**Maana:** kakamaa mwili kwa kutumia nguvu za misuli ya mwili wako kama ufanyavyo unaposukuma haja kubwa. |
| 5. | **Kita**<br>**Maana: i.** chomeka kitu kwa nguvu agh. juu ya ardhi k.v. mkuki.<br>**ii.** kuwa madhubuti katika jambo fulani. | **Jikita**<br>**Maana: i.** shughulisha sana akili yako katika jambo.<br>**ii.** kuzama kwa kifaa au zana mahali. |

**Chanzo:** Data ya KKS3 na KKK2 (2018)

Vitenzi vya Kiswahili katika Jedwali Na. 8 vinaonesha utabirifu wa kisemantiki kutokana na mazingira ya kisemantiki. Vitenzi hivyo vinaonesha kuwa, upachikaji wa mofimu {ji-} humsaidia msomaji kuweza kutabiri maana ikiwa anafahamu maana ya kitenzi ambacho hakina mofimu hiyo. Hii inatokana na ukweli kwamba dhana inayopatikana katika kitenzi ambacho hakina mofimu {ji-} ndiyo ambayo inaonekana katika kitenzi kilichopachikwa mofimu hiyo japokuwa dhana ya kitenzi chenye mofimu {ji-} huonesha kujirejelea kwa mtenda wa jambo.

## 5.0 Hitimisho

Makala haya yameelezea kwa ufupi utabirifu wa kisemantiki unaoweza kufanywa na mofimu {ji-} katika vitenzi vya Kiswahili kwa kuchunguza lugha ya Kiswahili na Kiingereza ili kuona kama hali inayojitokeza katika Kiingereza huweza kujitokeza pia katika Kiswahili. Matokeo yamebainisha mbinu mbili zinazoweza kudhihirisha vitenzi vya Kiswahili vyenye mofimu {ji-} katika KKS3 na KKK2,

yaani mbinu ya kileksikografia na mbinu ya ujazo wa kisemantiki. Pia, licha ya mofimu {ji-} kupachikwa katika baadhi ya vitenzi vya Kiswahili, si vitenzi vyote vilivyopachikwa mofimu hiyo husababishiwa utabirifu wa maana katika kitenzi hicho kutokana na kuwapo kwa mofimu hiyo. Kwa mantiki hiyo, madai yaliyotolewa na McCarthy (2002) kwamba mofimu moja inapopachikwa kabla ya shina la kitenzi katika vitenzi tofauti huweza kuonesha au kuwa na dhima sawa katika vitenzi vyote katika lugha ya Kiingereza hayafanyi kazi katika lugha ya Kiswahili kutokana na matokeo yaliyopatikana. Aidha, kuna mazingira yanayosababisha baadhi ya vitenzi vya Kiswahili vinapopachikwa mofimu {ji-} kuwa na utabirifu wa kisemantiki ilhali vitenzi vingine vinapopachikwa mofimu hiyohiyo kutokuwa na utabirifu huo. Mazingira hayo ni: mazingira ya kimofolojia na mazingira ya kisemantiki. Kwa kuwa makala haya yamechunguza mofimu tegemezi mojawapo na kuacha mofimu nyingine, mathalani, mofimu {-si-}, {-ku-} n.k. inapendekeza kwamba mofimu tegemezi nyingine ambazo hazijafanyiwa utafiti wa kina hususani kuhusianisha na semantiki zichunguzwe ili kubaini kama zina dhima moja tu au zaidi.

## Marejeleo


BAKITA (2015) *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (Toleo la Pili). Dar es Salaam: Longhorn Publishers (T) Ltd.

Katamba, F. na Stonham, J. (2006) *Morphology*. (Toleo la Pili): PALGRAVE MACMILLAN.

Khamisi, A.M. (1985) *Swahili Verb Derivation.* Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Hawaii, Hawaii.

Kreidler, C.W. (2002) *Introducing English Semantics.* London: Taylor & Francis e-Library.

Lieber, R. (2009) *Introducing Morphology*. Cambridge: Cambridge University Press.

Massamba, D.P.B. (2009) *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

McCarthy, A.C. (2002) *An Introduction to English Morphology: Words and their Structure.* Edinburg: University Press Ltd.

Mgullu, R.S. (1999) *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.

Rubanza, Y.I. (1996) *Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

TUKI. (2014) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (Toleo la tatu)*. Nairobi: Oxford University Press.

Wesana-Chomi, E. (1989) *Sarufi Tangulizi ya Kiswahili (Sarufi Maumbo).* Sebha: Idara ya Uchapaji Taasisi ya Lugha Sebha.